



The Tanganyika Law Society

The Bar Association Of Tanzania Mainland

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
17 Oktoba, 2010

Tume ya Uchaguzi imekitunukia Chama cha Mwakili cha Tanzania Bara (kwa kifupi "Chama") hadhi ya uangalizi wa Uchaguzi Mkuu ujao. Kwa mara ya kwanza Chama kitasambaza wanachama wake katika mikoa kumi ya Tanzania Bara yote ili kushiriki uangalizi wa vituo vya uchaguzi, pia kufuatilia mchakato mzima wa kampeni za uchaguzi.

Chama hiki ni Chama cha Wanasheria wa Tanzania Bara. Kama jukumu lake Chama kinatetea mfumo wa jamii ambapo haki na sheria vinaheshimiwa. Shabaha kuu ya Chama kipindi kinachoelekea Uchaguzi Mkuu ni kwamba uchaguzi ufanyike kwa utaratibu unaokidhi utawala wa sheria na unaoshahibiana na viwango bora na uzoefu wa kimataifa.

Kwa usemi wa Rais wa Chama, Bwana Felix George Kibodya, "Ni msimamo wetu kwamba matakwa ya wananchi yawe msingi wa mamlaka ya serikali. Jambo hili ndiyo mwanzo na hatima ya usimamizi wetu wa uchaguzi mkuu ujao".

Kwa lengo hili Chama kimeandaa 'Ilani ya Uchaguzi' inayofafanua shabaha na mchango wa Chama chetu kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ujao wa tarehe 30 Oktoba 2010. Shabaha zinazotajwa zitaweka misingi ya mchakato wetu wa ufuatiliaji na uangalizi.

Siku ya Uchaguzi kila mwangalizi atafuatilia shughuli zinavyoendelea katika vituo vya uchaguzi. Hususan, atafuatilia matukio ya ukiukaji wa taratibu za upigaji kura, usalama na hujuma kwa makasha ya kura, hitilafu za kuhesabu kura na uandishi wa matokeo.

Wanachama wetu watasambazwa Tanzania Bara katika mikoa 10 ifuatayo, yaani mikoa ya Tanga, Arusha, Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam, Tabora, Mbeya, Kilimanjaro, Mtwara na Mara.

Baada ya mkakati wa uangalizi, Chama kitatangaza kwa faida ya umma taarifa ya tathmini.

